

Jarida la

Toleo Na. 4

# SAMIA TENA

03/09/2025

2025-2030



# TUNDUMA

Yafurika Kampeni  
za Samia





## RAIS SAMIA KUTEKELEZA MAMBO MATANO KUMALIZA MSONGAMANO WA MAGARI BARABARA YA TUNDUMA

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema serikali yake itahakikisha inaondoa Msongamano wa Magari katika barabara ya Tunduma ili kukuza uchumi na kuokoa muda unaopotea wakati wa usafirishaji wa Mizigo.

Akiongea wakati wa kampeni mkoani Songwe, Rais Samia amesema msongamano wa magari umesababishwa na uboreshaji wa bandari ya Dar es salaam ambayo kabla ya maboresho hayo ilikuwa inahudumia tani milioni 15.8 na sasa inahudumia tani milioni 28.

Rais Samia amesema kutokana na ongezeko hilo barabara ya Tunduma pekee kwa sasa inapitisha tani milioni tisa kutoka milioni takribani nne za zamani.

Kutokana na ongezeko hilo, Rais Samia amesema serikali yake itahakikisha inafanya mambo makubwa matano ili kumaliza msongamano huo wa magari ambao umekuwa kero na kikwazo cha ukuaji wa uchumi kwa muda mrefu.

Mosi, serikali imeanza kupanua barabara ya Tanzania Zambia (TANZAM) kutoka Igawe hadi Tunduma kwa kiwango cha kilometa 75 ili iwe ya njia nne kubwa.

Pili, amesema serikali itaanza kukarabati Reli ya TAZARA ili kuweza kusafirisha mzigo mkubwa kwa njia hiyo.

Tatu, Serikali itajenga bandari kavu yenye ekari 1800 Katenjile kata ya Mpenja na kuongeza kuwa mkandarasi ameshapatikana.

Nne, amesema ataongeza barabara mbadala maeneo ya Mwakabange na Kisesa ili kuhakikisha usafiri unakuwa mzuri na wa haraka.

Tano, Rais Samia amesema wapo katika mazungumzo ya wenzetu wa serikali ya Zambia kuhakikisha mamlaka ya mapato ya huko inafanya kazi masaa 24 kama ilivyo Tanzania ili kuharakisha upitishaji wa Nyaraka na kuokoa muda unaopotea mpakani.

## RAIS SAMIA KUWASHA UMEME VITONGOJI VYOTE NCHINI

Mgombea Urais Kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kila kitongoji nchini kitapata umeme wa uhakika akichaguliwa katika kipindi chake cha pili.

Akiongea mkoani Songwe leo wakati wa kampeni, Rais Samia amesema,

“Vijiji vyote nchini vimeshapata umeme na vitongoji vichache. Nitahakikisha vitongoji vyote vinapata umeme”, amesema.

Kulingana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 vijiji vilivyounganishwa na huduma ya umeme nchini imeongezeka kutoka vijiji 8,587 mwaka 2020 hadi vijiji 12,318 mwaka 2024 sawa na asilimia 100.

Aidha, vitongoji 33,657 kati ya 64,359 vimeunganishwa na umeme sawa na asilimia 52.3. Pia kumekuwapo na ongezeko la kiwango cha kaya zilizounganishwa katika huduma ya umeme hadi kufikia asilimia 78 mwaka 2024 kutoka asilimia 39.9 mwaka 2020.





## RAIS SAMIA: SERIKALI KUGHARAMIA MATIBABU KWA WASIOJIWEZA TU

Mgombea Urais Kupitia Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema serikali yake itabeba mzigo wa matibabu kwa wale wasiojiweza tu na sio kila mtu.

Rais Samia amesema hayo wakati wa kampeni zake mkoani Songwe leo Septemba 3, 2025.

Rais Samia amesema, “Wakati nazindua kampeni kuna watu hawakunielewa, nilisema serikali itagharamia matibabu kwa magonjwa makubwa kwa wale wasiojiweza tu na sio kila mtu”.

Rais Samia ameongeza kuwa kuna maeneo mengine wanasema itakuwa kwa kila mtu sio kweli bali ni kwa wale wasiokuwa na uwezo ili afya zao ziimarike na maisha yao yaendeleo.





## **SERIKALI KUJENGA MRADI MKUBWA WAKUSAFIRISHA UMEME KUTOKA IRINGA HADI ZAMBIA**

Mgombea Urais Kupitia Chama Cha Mapinduzi ( CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuhakikisha kila kitongoji nchini kinapata umeme wa uhakika akichaguliwa katika kipindi chake cha pili.

Akiongea mkoani Songwe leo wakati wa kampeni, Rais Samia amesema, “Vijiji vyote nchini vimeshapata umeme na vitongoji vichache. Nitahakikisha vitongozi vyote vinapata umeme”, amesema.

Kulingana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 vijiji vilivyounganishwa na huduma ya umeme nchini imeongezeka kutoka vijiji 8,587 mwaka 2020 hadi vijiji 12,318 mwaka 2024 sawa na asilimia 100.

Aidha, vitongoji 33,657 kati ya 64,359 vimeunganishwa na umeme sawa na asilimia 52.3. Pia kumekuwapo na ongezeko la kiwango cha kaya zilizounganishwa katika huduma ya umeme hadi kufikia asilimia 78 mwaka 2024 kutoka asilimia 39.9 mwaka 2020.



## VWAWA WAAHIDI MITANO TENA KWA SAMIA

Mgombea wa Nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Vwawa mkoani Songwe kwa kunadi sera na ahadi zake katika kuomba kura ili kuendelea kuongoza Taifa la Tanzania, leo tarehe 3 Septemba 2025.

Dkt. Samia ametoa shukrani kwa wananchi wa Vwawa kwa kujitokeza kwa wingi hali ambayo imezidi kumtia moyo na nguvu kubwa katika kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Nao wananchi wa Vwawa wamemtoa shaka Dkt. Samia kwa kumthibitishia kwa kauli moja kwenda kufanya maamuzi sahihi siku ya tarehe 29 Oktoba kwa kumpa kura nyingi za ndio ili kupata ushindi mnono na wa kishindo.





## RAIS SAMIA: KILA MTANZANIA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA

Mgombe Urais Kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema iwapo wananchi watampa ridhaa ya kuongoza tena kwa kipindi cha miaka mitano, serikali yake itahakikisha kila mtanzania anapata maji safi na salama.

Rais Samia amesema hayo leo wakati akihutubia maelfu ya wananchi Tunduma, Mkoani Songwe. Ameongeza kusema ilani ya CCM inamtuma kuhakikisha kila mtanzania anapata maji safi na salama.

Kulingana na Ilani ya CCM ya mwaka 2025 kumekuwapo na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kutoka asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 79.6 na kwa mijini kutoka asilimia 84 hadi asilimia 90 mwaka 2024.

Ongezeko hilo limechangiwa na kukamilika kwa ujenzi wa miradi 1,633 ya usambazaji maji mijini na vijijini iliyowanufaisha jumla ya wananchi 12,547,526.



# WASANII WAIBUA SHANGWE KAMPENI ZA CCM







## SAMIA SIRI YA UKANDA WA NYANDA ZA JUU KUSINI KUZALISHA CHAKULA KWA WINGI

Katibu Mkuu mstaafu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ambaye pia ni mgombea ubunge kwa Jimbo la Makambako, anasema uamuzi wa Rais Samia, kuweka pembejeo na ruzuku kumeleta tija kwenye kilimo kwa Ukanda wa Nyanda za juu Kusini na kumepelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi.

"Mwaka 2021 hatukuwa na ruzuku za pembejeo za kilimo lakini ni Rais Samia kwa uamuzi wa busara na mapenzi yake wakulima wa nchi hii alifanya uamuzi mkubwa wa kutoa pembejeo kwa wakulima ili wananchi wasibebe mzigo huo.

"Mhe. Rais Samia alibeba jukumu la kutupatia pembejeo na ruzuku na sisi tukabakia na jukumu la kulima na kuzalisha tu, nani kama Samia?, " alihoji.

Katika eneo la afya, anasema wananchi wa jimbo hilo wanapata tiba kwenye kila kona na kuainisha kuwa katika kila wilaya Mhe. Rais amepeleka huduma za dhararura (emergency services) kwa kuwa na jengo lake maalumu.

Aidha, kwenye eneo la elimu Mhe. Rais Samia ametoa elimu bure kwa wanafunzi wa shule za msingi mpaka sekondari kidato cha sita.

"Pia, katika eneo la barabara, ukienda Isongole - Ileje, umetuletea zaidi ya bilioni 70 ili kutuunganisha na upande Kyela mkoa wa Mbeya, " anasema.



## BALOZI NCHIMBI AUNGURUMA LALAGO - MASWA

Mgombea Mwenza wa CCM, Balozi Emmanuel Nchimbi, akizungumza na wananchi wa Lalago - Maswa katika mkutano wa hadhara.

Amewasilisha Ilani ya CCM 2025-2030, akieleza mafanikio yaliyopatikana Maswa chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuahidi maendeleo mapya yatakayogusa maisha ya kila mkulima, mfugaji, kijana na mfanyabiashara.

Maswa imeahidi kutiki Oktoba kwa Daktari Samia Suluhu Hassan.





## KISHAPU YAFANA, BALOZI NCHIMBI APANDISHWA CHEO

Watemi wa Shinyanga wamempandisha cheo Balozi Emmanuel Nchimbi kuwa Ng'wambheleja, msaidizi wa Chifu Hangaya (Dkt. Samia).

Amepewa jina la heshima Jiluguya Mayela - msafisha njia wa Chifu. Hii ni baraka za kimila kuelekea ushindi wa CCM 2025.





## **RAIS SAMIA: VETA MALIPO NI KWA SERIKALI, VIJANA WAPATE UJUZI**

Mgombea wa Nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa katika awamu yake ya uongozi Vijana watakaosoma vyuo vya ufundi hawatalipa ada.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati akihutubia maelfu ya wananchi Vwawa Songwe wakati wa kampeini za kuomba ridhaa ya kuongoza tena miaka mitano.

Rais Samia amesema, “Tunajenga VETA vijana wapate ujuzi. Malipo yatakuwa kwa serikali kama tunavyofanya shule za msingi hadi sekondari”

Rais Samia amesema elimu ya ya VETA sasa inaenda kuingia katika mpango wa serikali wa kutoa mikopo kwa vijana.







## KONA YA ILANI

Dondoo kutoka katika Ilani 2025 kwa Tanzania: Kuchochea mapinduzi ya uchumi wakisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasilimali zinazozalishwa nchini;

# KTORBA



# KUFAKILI



*Kazi na Utu  
Tunasonga Mbele*

ssh\_anatekeleza